

Jina.....
Shule.....

Nambari yako.....
Sahihi yako.....
Tarehe.....

102/2
KISWAHILI
LUGHA
KARATASI YA 2
Julai/Agosti 2012
Muda: Saa 1 $\frac{3}{4}$

JARIBIO LA TATHMINI YA PAMOJA WILAYA YA BUTULA – 2012
Kenya Certificate of Secondary Education (K.C.S.E)

102/2
KISWAHILI
LUGHA
KARATASI YA 2
Julai/Agosti 2012
Muda: Saa 1 $\frac{3}{4}$

SWALI	AFAHAMU	ALAMA
1	UFUPISHO	
2	MATUMIZI	
3	MATUMIZI YA LUGHA	
4	ISIMU JAMII	
JUMLA	80	

*Karatasi hii ina kurasa 2 zilizopigwa chapa
Watahiniwa wanastahiliku hakikisha kuwa maswali yote yako na hakuna yaliyoachwa*

UFAHAMU:

1. Soma makala haya kisha ujibu maswaliyanayofuata.

Mojawapo ya athari kubwa katika “maendeleo ya jamii za kisasa” ni kupapia tamaduni za kimagharibi na kutupilia mbali tamaduni ambazo toka jadi zimekuwa mlezi wa jamii nyingi barani Afrika. Ni muhimu kutambua kuwa hakuna utamaduni ambao umeustawisha mwingine. Badala ya kuimarisha utamaduni dhaifu na kuupa nguvu, utamaduni wenyewe nguvu huumeza na kuuangamiza ule dhaifu. Ingawa wengi huona upapiaji wa utamaduni wa kigeni kama ustaaraba na maendeleo, hali hii huwa na athari hasa kwa wanaotupilia mbali tamaduni zao.

Athari kubwa ni katika uwanda wa lishe. Lishe ni sehemu ya utamaduni wa watu. Jamii ya watu inapofikia uamuzi wa kuwa nyama ya nyoka, na wala si ya ngombe, iwe sehemu ya chakula katika utamaduni wake, huwa imefanya uamuzi huu kwa uangalifu mkubwa.

Aghalabu, wavyele wa jamii za Kiafrika walifikia kuwa na vyakula ambavyo havikuwa vya kujaza tumbo tu na kuharibu mwili. Vilikuwa vyakula ambavyo vilinawirisha mwili huku vikitumika pia kama dawa ya kuutibu mwili huo. Wala si mwili tu. Viliweza pia kujali mazingira, kwani vingi vilizuia mmegeko wa udongo na pia kuongezea rutuba na virutubishi muhimu katika udongo.

Moja ya chakula cha jadi kwa jamii nyingi za Kiafrika kilikuwa na manufaa lukuki kama lishe na mmea. Wataalamu wa lishe wanasema kuwa kiasi cha kikombe kimoja cha juisi ya viazi vitamu huupa mwili kiwango cha vitamini E kinachohitajika kwa siku. Kiazi kitamu kimoja nacho huupa mwili asilimia sitini na tano ya kiwango cha madini ya vitamini C. Vitamini hizi ni muhimu sana kwani huukinga mwili kutokana na uharibifu wa seli. Kinga hii huzuia mwili kukonga kwa haraka huku ikiimarisha kingamwii na kuzuia uwezekano wa kupata mtoto wa jicho, maradhi ya saratani ya matiti au ya tezi inayozungukia shingo ya kibofu cha mkojo kwa wanaume.

Viazi vitamu vimesheheni pia madini yaliyo muhimu kwa mwili. Mathalani, vina madini ya shaba ambavo hudumisha uzima wa vifundo na kulainisha ngozi na madini ya manganizi yanayodumisha uzima wa mifupa pamoja na kuvunjavunja na kugeuza wanga, protini pamoja na mafuta kuwa kawi inayohitajika na mwili kuupa joto. Manganizi pia husaidia katika utumaji wa ujumbe kwenye misuli ili iweze kulegea au kukazika. Viazi hivi vilevile vina madini ya fosforasi ambayo ni muhimu kwa afya na udhabitwa mifupa na meno. Madini haya pia huimarisha kukua kwa seli za mwili na kukarabati zile ziizoathirika na zilizo dhaifu.

Licha ya wingi wa madini, kiazi kitamu kinasifikasi kuwa na wingi wa utembwe ambao ni adhimu mwilini. Utumbwe husaidia kudhibiti ongezeko la uzani na kuimarisha utendakazi wa matumbo. Halikadhailka, madini hayo huzuia uwezekano wa kupata maradhi ya moyo. Ulaji wa viazi vitamu hupendekezwa sana na wataalamu wa lishe kwa wagonjwa wa bolisukari kutokana na uwezo wa madini haya wa kudhibiti kiwango cha sukari mwilini. Wataalamu wawa hawa husifia jinsi viazi vitamu humeng’enywa polepole na kwa utaratibu ikiinganishwa na viazi vingine, hali wanayosema huinua kiwango cha sukari mwilini kwa utaratibu na hivyo kudumisha kiwango kinachohitajika cha insulinii.

Viazi vitamu vinaweza kuliwa vikiwa vibichi. Vilevile, vinaweza kupikwa aidha kwa kuokwa au vikakaushwa katika mafuta moto na kuliwa kama chipsi au vikachemshwa na kuliwa vizimavizima, au kama vimepondwapondwa. Hupendekezwa kuwa vyakula ambavyo vinaweza kuliwa vibichi viliwe vile, kwani vina manufaa mengi kuliko vilivypikwa. Hii ni kwa kuwa virutubishi vingi hupotea vyakula vinapopikwa.

Hii kupunguza baadhi ya changamoto za kiafya tunazoshuhudia leo hii, itakuwa muhimu kuhamasisha umma kuasi maendeleo pofu na kurejelea vyakula vyetu vyta kiasili. Vyakula hivi pia hustahimili hali mbalimbali za anga na hivyo kuwa suluhu kwa tisho la jaa.

Wasiojua basi washike shauri kuwa vyakula wanavyokimbilia vyta magharibi kama pizza, hambaga na soseji vina madhara mengi na kwamba vyakula vyta kiasili ndio mhimi wa afya na uzima.

Maswali

- a) Mwandishi anasema lishe inaathiri vipi utamaduni wa wato? (al 2)
- b) Mwandishi ana maoni gani kuhusu maendeleo.
- c) Wavyele walifikia uamuzi kuwa chakula hiki kiwe lishe yetu vipi. (al.3)
- d) Onyesha manufaa manne ya viazi vitamu. (al 4)
- e) Eleza matumizi ya maneno yafuatayo kulingana na taarifa.
 - i) Utembwe
 - ii) Mmegeko
 - iii) Hmeng'enywa
 - iv) Maendeleo pofu

Soma Makala haya kasha ujibu maswali yanaofuata.

Mawasiliano husemekana kuwa ndilo jambo muhimu zaidi baina ya wanadamu. Lakini, je, mawasijano ni nini?

Neno mawasijano iimeelezwa kwa njia mbalimbali na wataalamu tofautitofauti. Maana timiifu inayoonekana ni kuwa mawasiliano ni usafirishaji wa ama mbalimbali za ujumbe kutoka kwa mtu anayetuma ujumbe, ambaye anaweza kuwa mwanamume, mwanamke, mzee au mtoto hadi kwa vile apokeaye ujumbe huo popote pale alipo, iwe karibu au mbali, kwa kutumia nyenzo au njia fulani maalumu.

Nyenzo aina aina hutumiwa kuwasilisha ujumbe. Moja ya hizi ni zana zinazota sauti. Tangu jadi, Waafrika wamekuwa wakitumia baragumu kutuma taarifa. Katika jamii mbalimbali, watawala walitumia ngoma kuwakusanya watu. Aidha, ngoma ziitumiwa kuarifu matukio mema kama kuzaliwa kwa mtoto wa mfalme. Wakati mwengine zana hizo ziitumiwa kuonya juu ya hatari kama vile uvamizi. Methali 'Mbiu ya mgambo ikilia kuna jambo' ilisadifu kuelezea matumizi haya. Siku hizi kuna zana na sauti za aina nyingi zinazotimiwa kutoa ujumbe.

Nyenko nyingine inayotumiwa kupidisha ujumbe ~~au~~ ishara na miondoko ya mwili. Kukonyezajicho hutumiwa kumaanisha jambo fulani, huku kutikisa kichwa hudhihirisha maana nyingine kutegemea jamii na mazingira hata vitendo kama kurusha mikono au mtu kusogea huwa na maana kwa wanaohusika.

Kama ilivyodokezwa hapo juu, kuna nyenko nyingi za mawasiliano. Lakini iliyo muhimu zaidi ya zote ni lugha. Kutokana na sauti zitolewazo kupidia ala za sauti, binadamu huweza kupidisha ujumbe wa namna mbalimbali.

Kila sauti, iwe ya irabu ~~au~~ konsonanti, huwa na maana maalumu. Sauti hizi zikiunganishwa kwa mpangilio maalumu ~~hufoa~~ ujumbe fulani.

Mawasiiano hutekeleza majukumu anuwai katika jamii, hasa lugha inapotumiwa. Lugha ni chombo cha kimsingi katika kuelezea'hisia kutoka kwa mtu mmoja hadi kwa mtu au watu wengine. Yaani, lugha ndio hutumiwa kuwasiiha mapenzi, furaha, umoja, huruma, woga, wasiwasi, uhasama, chuki au utengano. Kupitia kwa hisia zipitishwazo kwa lugha, watu huweza kufarakanaau kutangamana.

Wanadamu huwasiliana iii kuendeleza mahusiano. Hii ni sifa ya mwanadamu ambayo wanyama hawakubahatika kupewa. Hivyo basi, bila lugha ambayo pia ni kipawa alichotunukjwa binadamu peke yake, watu hawawezi kuingiliana wala kujenga uhusiano.

Kupitia kwa mawasiliano, tunatimiza wajibu wa kijamii. Utamaduni wa Mwfrika unadai kuwa watu wakutanapo yapasa waamkiane, wajuliane hali, watambulishane na watakiane heri. Mambo haya huwa ni ishara ya amani. Kimya huchukujwa kama utovu wa adabu au hatua ya kutangaza uhasama na hata vita.

Halikadhajika, mawasiliano kupidia kwa lugha hutekeleza dhima moja ya kimsingi katika jamii: kuelimisha wanajamii, Lugha hutumiwa kupidisha rnaanifa, stadi, mielekeo na maadili kutoka kizazi kimoja hadi kingine.


Mambo haya ndio msingi wa kudumisha na kuendeleza jamii. Bila mawasiliano, huenda wanadamu wangkuwa wameangamia jinsi ama fulani za viumbe kama Dodo walivyofutika kutoka uso wa dunia.

Maswali

2. Ufupisho (Alama 15)
-
-
-
-
-
-
-
-
-
-
-
-
-
-
-
-
-
-
-
-
-
-
-
-
-
-
-
-
-
-

Maswali

- b) Eleza ujumbe uliomo katika aya ya 3,4,5, na 6 (Maneno 50) (al 7)
Nakala chafu.



Nakala safi

- b) Pambuu majikumu ya mawasiliano kama yanavyojoitokeza katika kifungu (maneno 50) (al 6
Nakala Chafu (Mtiririko al.1)

Nakala safi

Matumiziya hifha (alama 40)

3. a) Eleza kwa kutolea mfano tofauti kati ya ala tule na ala sogezi. (al.4)
-
.....
.....
.....
- b) Taja irabu ambayo hutumika kati na mbele ya ulimi (al.1)
-
.....
.....
.....
- c) Tunga sentensi kubainisha ngeli ya jina hili chetezo. (al.2)
-
.....
.....
.....
- d) Eleza matumizi matatu ya italiki kisha tolea mifano kwa kila aina. (al 3)
-
.....
.....
.....
- e) Tunga sentensi ukitumia kitenzi kifuatacho katika kauli ya kutendeka - la (al- 2)
-
.....
.....
.....
- f) Bainisha vielezi katika sentensi zifuatazo kasha uleze ni vya aina gani. (al.4)
-
.....
.....
.....

- i) Atakapomaliza kudurusu ~~mwachilie~~ (al.4)

ii) Tukitembea kwa kasi tutaliwahi basi.

g. Chagua ukitumia kielezo matawi.

Yule Semenza wa Afrika Kusini ni mjuzi kuliko wengine.

h) Tunga sentensi ukitumia kirai kihuishi. (al.2)

i) Kanusha

Kuliko na kiangazi kwahitaji msaada. (al 2)

j) Bainsha matumizi ya yambwa na chagizo katika sentensi (al.2)

Alimtupia kalamu jioni kwa mkono

k) Geuza katka usemi wa taarifa

“Kwa nini unamrudi mtoto mdogo?” afisa wa maslahi ya mototo aliuliza.

-
.....
.....
- l) Andika kwa udogo
Wahisani wamewajengea mifango ya kuitia. (al.2)
-
.....
.....
- m) Tunga sentensi moja kudhihirisha tofauti ya maneno haya. (al 2)
-
.....
.....
- n.) Andika kitenzi kimoja (al 2)
i) Asili ya kigeni
.....
.....
.....
.....
ii) Asili ya kigeni
.....
.....
.....
.....
- o) Eleza matumizi ya kwa katika sentensi ifuatavyo Rabima alitembea kwa utaratibu kwa kutaka
kuepuka kuanguka ,matopeni alipokuwa akija kwetu.
-
.....
.....
.....
- p) Eleza maana mbili ya sentensi hii (al2)
Shamba letu limelimika
.....
.....
.....
.....

- q) Andika kisawe cha bara – bara (al.1)

ISIMU – JAMII(ALAMA 10)

1. Taja na ueleze dhima tano ambazo sajili za lugha tofauti hutekeleza. (al 10)

